

JA, KIGEZO CHA DUS NI NINI?

DUS inasimamia **bainifu, inayofanana** na **thabiti**. Ili aina ya mbegu iingizwe katika Orodha ya Aina ya Mbegu, lazima ifikie kigezo cha DUS.

- ❶ **Bainifu/ya kipekee** inamaana kuwa aina ya mbegu *isifanane* na aina nyingine za mbegu.
- ❷ **Inayofanana** inamaana kuwa aina ya mbegu lazima izalishe mimea ambayo inafanana – katika urefu na rangi – kutoka msimu moja hadi nyingine.
- ❸ **Thabiti** inamaana kuwa aina ya mbegu haitabadilika inapopandwa msimu baada ya msimu.

Hata hivyo, wakulima wadogo hupanda mbegu ambazo sio bainifu/ya kipekee, zisizofanana, au zisizo thabiti. Wanahitaji aina mbalimbali ya mbegu ambayo inaendana na mazingira yao na inakidhi mahitaji ya soko ya ndani. Kwa hiyo, aina mbalimbali za mbegu wanazozalisha haziwezi kufikia kigezo cha DUS.

ATHARI ZA KIGEZO CHA DUS KWA WAKULIMA WADOGO

Kigezo cha DUS kinatengeneza aina ya mbegu inayofaa kwenye kilimo cha mazao ya aina moja na inayotumia kemikali za viwandani kwa ajili ya kilimo. Hii haina manufaa kwa wakulima wengi barani Afrika, ambao ni wakulima wadogo, wanaohitaji kupanda mimea ya aina mbalimbali na ambao hawawezi kumudu mbolea ghali za viwandani.

Kigezo cha DUS kinalenga kusambaza aina moja ya mbegu katika mifumo ya kilimo cha viwanda na biashara kwa kiasi ambacho kitadhoofisha aina ya mbegu zilizoendelezwa na wakulima wadogo kwa vizazi.

Inakadiriwa kuwa angalau asilimia 75 ya aina mbalimbali ya mimea duniani imepotea kwa sababu wakulima wametelekeza mbegu zao za asili kwa ajili ya mbegu zinazofanana (k.v. DUS).

Kabla ya DUS...



Baada ya DUS...

